**KAMPENI YA UHURU WA KUJIELEZA NA UHURU WA KUKUSANYIKA**





**“BILA UHURU WA KUJIELEZA NA KUKUSANYIKA HATUWEZI KUENDELEA”**

# Tamko la wadau juu ya kampeni ya kulinda Uhuru wa Kujieleza na Uhuru wa Kukusanyika

Kampeni ya pamoja ya kulinda Uhuru wa Kujieleza na Uhuru wa Kukusanyika imezinduliwa rasmi leo na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kupitia mradi wa UHAKIKI kwa kushirikiana na wadau washirika wengine 8 ambao ni Policy Forum, Twaweza, TGNP, Tanzania Center for Democracy, WiLDAF, Baraza la Habari, Jukwaa la Wahariri na Tume ya Haki Za Binadamu na Utawala Bora.

Kampeni hii inaangazia mambo makuu yanayogusa na kuibua mijadala juu ya haki za kiraia na haki za kisiasa nchini Tanzania. Kauli mbiu ya kampeni hii ni “Bila uhuru wa kujieleza na kukusanyika hatuwezi kuendelea”

## Uhuru wa Kujieleza

Msingi mkuu wa dhima ya vyombo vya habari katika kushajiisha uhuru wa kujieleza ni dhana ya demokrasia. Dhana ya demokrasia imekuja kujulikana sana duniani kama utawala wa watu, kwa ajili ya watu unaoendeshwa na watu wenyewe. Moja ya nguzo kuu za demokrasia ni uwepo wa

uhuru na haki ya wananchi kuwa na maoni na kujieleza. Uhuru huu kimsingi huenda sambamba na uhuru wa vyombo vya habari na haki ya kutafuta na kupokea taarifa.

Hapa nchini Tanzania uhuru wa kujieleza unalindwa na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 katika Ibara ya 18. Sambamba na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzani, ipo mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo inalinda uhuru wa kujieleza, mikataba hiyo inajumuisha:

- ***Tamko La Ulimwengu La Haki Za Binadamu*** (Universal Declaration of Human Rights 1948) pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Haki za Watu. Ibara ya 19 inatoa haki na uhuru wa kila mtu kuwa na maoni yake na kujieleza na bila mawasiliano yake kuingiliwa .
- Mkataba Wa Afrika Wa Haki Za Binadamu Na Watu (*The African Charter on Human and People's Rights* (1981)
- Tamko La Kanuni Za Uhuru Wa Kujieleza Afrika (*Declaration of Principles on Freedom of Expression in Africa)*

Haki ya Uhuru wa kujieleza nchini inakabiliwa na changamoto kadhaa, tangu kupitishwa kwa sera ya utangazaji nchini Mwaka 1993, sheria nyingi zilizotungwa zimekuwa zikikinzana na Katiba pamoja na mikataba ya kimataifa juu ya uhuru wa kujieleza. Katika kipindi cha hivi karibuni, tangu mwaka 2015 hadi sasa, kumekuwepo na utungwaji wa sheria zinazodhoofisha uhuru wa kujieleza nchini Tanzania. Sheria hizo ni Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015, Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka, 2016 pamoja na Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya mwaka 2015. Hivyo Kampeni imejikita zaidi katika kuongeza uelewa kwa jamii juu ya haki hizi mbili; haki ya kujieleza na haki ya kukusanyika.

Sheria ya Takwimu inazuia mijadala juu ya usahihi wa takwimu, inazuia watu na taasisi kuchapisha taarifa zao wenyewe, na kuyumbisha uhuru wa kujieleza kwa kuwatisha watu kwa adhabu ya kifungo na kulipa faini.

Uwanda wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ni mpana sana na haujitoshelezi kwa kulinganisha na mahitaji ya vyombo vya habari, huduma za vyombo vya habari, na machapisho. Tafsiri ya mwandishi wa habari pia haijitoshelezi kwani inaweza kuwajumuisha waandishi wa

*blogu* na watu wanaochapisha ujumbe kupitia mitandao ya kijamii. Kuna shaka kwamba utoaji wa leseni na kuthibitisha waandishi utasababisha mipaka isiyo na msingi kwenye uhuru wa kujieleza.

Mfumo wa kuwathibitisha na kuwapa vyeti waandishi unakinzana na viwango vya kimataifa. Katika tamko la pamoja la tume maalumu ya Uhuru wa Maoni na Uhuru wa Kujieleza ya Umoja wa Mataifa la mwaka 2003 linaweka wazi kwamba waandishi wa habari hawatapaswa kusajiliwa wala kuadhinishwa na hakupaswi kuwepo kwa vizuizi vya kisheria juu ya nani anaweza kuwa mwandishi wa habari. Sheria hii ianapelekea vikwazo vinavyoingilia uhuru wa wahariri.

Sheria hii pia inafanya kitendo cha uchapishaji taarifa inayosemekana kuwa ya uongo, kuwa ni kosa.

Kwa upande wa Sheria ya Makosa ya Mitandaoni madhaifu makubwa yapo katika kosa la kuchapisha taarifa za uongo. Neno taarifa katika Sheria hii lina tafsiri pana sana. Sheria hii tayari imeshakuwa mwiba kwa baadhi ya watu ambao wamefunguliwa mashitaka kwa kwa kutoa maoni yao katika makundi ya WhatsApp na kurasa binafsi za facebook na pia wafanyakazi 36 wa LHRC walishawahi kukamatwa kwa kudaiwa kukusanya na kusambaza matokeo ya uchaguzi.

Ripoti ya Mtazamo wa Haki za Kisiasa na Kiraia iliyotolewa na LHRC mwaka 2016, inaonyesha kuwa haki ya kujieleza imepata alama C ambayo ni chini ya wastani.

Katika kukabiliana na hali hii kama wadau, tunapendekeza kupitiwa na kuzifanyia marekibisho ili kuhakikisha kwamba zinaendana na Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo taifa limeridhia.

## Uhuru wa Kukusanyika

Ndugu wanahabari, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua umuhimu wa haki ya kukusanyika na ndio maana ikajumuishwa katika Katiba yetu ya mwaka 1977. Katika Ibara ya 20(1) ambayo inasema *"kila mtu ana haki ya kukusanyika kwa uhuru na amani, kujihusisha na kushirikiana na watu wengine, kwa minajili hiyo kutoa maoni hadharani na kuunda na kujiunga*

*na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kulinda au kudumisha imani au maslahi yake mengine"*

Sambamba na Katiba, mikataba mingi ya kimataifa ya haki za Binadamu pia inasisitiza umuhimu wa kuwepo kwa uhuru wa kukusanyika husussani katika nchi za kidemokrasia. Hata hivyo ripoti mbalimbali ikiwemo Ripoti ya Mtazamo wa Haki za Kisiasa na Kiraia iliyotolewa na LHRC mwaka 2016, inaonyesha kuwa haki ya kukusanyika imekuwa mashakani ikitishiwa na kauli za viongozi, wanasiasa na jeshi la polisi. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, haki ya kukusanyika imepata alama D ambayo ni mbaya.

Sisi kama wadau tumeamua kuendesha kampeni hii baada ya kubaini Changamoto kadhaa zinazodunisha uhuru wa kukusanyika nchini. Baadhi ya Changamoto hizo ni kama zifuatazo:

1. Uzuiaji holela wa mikusanyiko: uzuiaji wa mikutano kwa kufuata busaza za wenye mamlaka umekuwa ukiongezeka siku hadi siku, viongozi kutumia mamlaka waliyonayo bila kuwa na sababu za msingi imekuwa kawaida katika uzuiaji wa mikusanyiko. Kuna takwimu chache za kiserikali nchini Tanzania kuhusiana na haki ya kukusanyika, ambapo inafanya kuwa vigumu kidogo kuelewa juu ya namna ya kutumia haki hii iliyobadilika kwa kipindi fulani. Asasi za kiraia na vyombo vya habari aidha wametoa taarifa kuhusu matukio ya jeshi la polisi kuzuia haki hii kiholela
2. Mkanganyiko wa sheria na majukumu: Licha ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Sheria ndogo ya mwaka 2002 kueleza taratibu ambazo jeshi la polisi wanapaswa kuzifuata katika kusimamia mikusanyiko na mandamano ya umma, maneno maandamano na mikusanyiko haijafafanuliwa kwenye sheria ya polisi. Sheria inasema kuwa mkusanyiko wa watu watatu au zaidi ambao hawatii amri ya kutawanyika wanapoambiwa na polisi, unaweza kutafsiriwa kama mkusanyiko usio halali. Hali hii inafanya uhuru wa kukusanyika kutawaliwa na utashi wa jeshi la polisi badala ya kubaki kuwa haki ya kikatiba.
3. Matumizi holela ya nguvu katika kutawanya makusanyiko: Sheria inatanabaisha kwamba serikali ina wajibu wa kuunga mkono uhuru wa kukusanyika kwa kuweka mazingira rafiki ikiwemo kuhakikisha wananchi wanakusanyika katika mazingira salama na tulivu na kwa amani, hata hivyo badala ya dola kuwajibika katika hili, kumekuwepo kwa matukio mengi yanayohusisha jeshi la polisi kutumia nguvu kupita kiasi na bila kuwajibishwa katika kuvuruga haki ya kukusanyika.

4. Kukosekana kwa utaratibu maalumu katika matumizi ya maeneo ya wazi: upatikanaji wa maeneo ya wazi ya umma ambayo mara nyingi yamekuwa yakitumika kwa mikusanyiko ya umma unaweza kuwa kikwazo kwa uhuru wa kukusanyika endapo kibali cha kutumia maeneo hayo kitakataliwa kwa nia ovu. Utaratibu unapaswa kuwekwa hasa kwa maeneo ya miji na majiji ambapo mikutano mingi huvuta hisia za watu wengi kutokana na uwepo wa vyombo vya habari.
5. Kukataliwa kukusanyika bila kuwajibika: Kama ilivyoelezwa hapo juu sheria inaruhusu mipaka ya mikusanyiko katika mazin
6. gira fulani. Huku ukiendelea kuzingatia sheria za nchi na masuala ya usalama vimetajwa na polisi kama ndiyo sababu ya kuzuia mikusanyiko, hakuna sababu maalumu zilizotolewa. Huwa ni siri 'vyanzo vya usalama' vimetajwa. Aidha uzuiaji wa mikutano hutolewa katika hali isiyo rasmi badala ya njia rasmi kwa maandishi. Zaidi ya hapo wananchi wana uelewa mdogo wa kukata rufaa dhidi ya kukataliwa, na wanaweza wasiwe na nia ya kukata rufaa kwenye mamlaka za juu ili kuwajibishwa, na ndiyo hunaonekana kuna usimamizi mdogo wa majukumu ambayo polisi anayo katika kupiga marufuku.

Katika kuboresha hali ya uhuru wa kukusanyika nchini, wadau tunapendekeza yafuatayo:

1. Serikali kulinda haki hii ya kikatiba ya kukusanyika, kwa kuimarisha ulinzi kwa wananchi wanapohitaji kukusanyika kwa ajili ya shughuli za kijamii hata shughuli za kisiasa na kiuchumi.
2. Sheria ya Jeshi la polisi na sheria ndogo zifanyiwe marekebisho ili maana ya neno mkusanyiko liweze kuendana na viwango vya kitaifa na kimataifa.
3. Jeshi la polisi kufuata sheria na kutumia busara katika kusitisha maandamano ya wananchi badala ya kutumia nguvu kupita kiasi. Jeshi la polisi linapaswa kuwa na mfumo thabiti wa kuimarisha ulinzi na Usalama pale wananchi wanapotaka kutekeleza haki yao ya kuandamana kama ilivyopambanuliwa katika Katiba.

Katika kampeni hii tunasisitiza serikali kufahamu umuhimu wa wananchi kujumuika katika kuleta maendeleo ya nchi kwa ujumla. Tunaamini kwamba watanzania hawawezi kuendelea bila kuwa na haki ya kukusanyika kwa uhuru na amani, kujihusisha na kushirikiana na watu wengine, kwa minajili hiyo kutoa maoni hadharani na kuunda na kujiunga na vyama au mashirika

yaliyoanzishwa  kwa madhumuni ya kulinda au kudumisha imani au maslahi yake mengine; kwani kwa kufanya hivyo wanaweza kujadili ajenda mbalimbali za maendeleo na kushauriana namna ya kusonga mbele kama taifa.

Imesomwa na:

Katibu Mtendaji, Baraza la Habari (MCT)

……………………………………

Mkurugenzi wa Utetezi na Maboresho,

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

………………………………………

Machi 1, 2017, Dar es Salaam Tanzania